

Chukua Msimamo Upande wa Ibada ya Kweli (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 16 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, WAKRISTO WA KWELI WANAPASWA KUWAAMBIA WENGINE KUHUSU IMANI YAO?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda baadhi ya watu wakasema ndiyo?

Kwa nini huenda baadhi ya watu wakajibu hapana?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

Wakristo wa kweli wanaepuka kubishana kuhusu imani za kidini.

(Ona sura ya 16 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 13-17.)

Soma Wakolosai 4:6.

Mstari huu unaonyeshaje kwamba tunahitaji kuwa na busara tunapowaeleza wengine kuhusu imani yetu?

Soma Mathayo 7:12.

Ikiwa wengine hawakubaliani na imani yetu, kwa nini tunapaswa kuendelea kuwaheshimu?



Unapocheza mchezo wa kurushiana mpira, unarusha mpira kwa njia ambayo mwingine ataweza kuudaka kwa urahisi. Vivyo hivyo, tunapaswa kueleza imani yetu kwa busara ili wengine waelewe maoni yetu

Wakristo wa kweli hukutana na waabudu wenzao ili kujifunza jinsi ya kuzungumza na watu wanaotaka kujua mambo mengi zaidi kuhusu imani yao.

(Ona sura ya 16 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 18-19.)

Soma Zaburi 22:22; Waroma 1:12; na Waebrania 10:24, 25.

Tunapata faida gani kutokana na kufanya mikutano kwa ajili ibada pamoja na Wakristo wenzetu?

Soma Malaki 3:10.

Tutapata nini ikiwa tutachukua msimamo upande wa ibada ya kweli?

Unaweza kumweleza *nani* mambo unayoamini, na unaweza kufanyaje hivyo kwa busara?



ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA...

Sikuzote Mashahidi wa Yehova mnajaribu kuwalazimisha watu wakubali imani yenu.

UNAWENZA KUSEMA HIVI...

Tunafurahi *kuwaeleza* imani yetu watu ambao wangependa kujua mambo tunayoamini. Lakini *hatumlazimishi* mtu yeyote abadili imani yake kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje aelewe andiko hilo?

MTU AKISEMA...

Dini ni jambo la kibinafsi, haipaswi kuzungumziwa na watu wengine.

UNAWENZA KUSEMA HIVI...

Hayo ni maoni ya kawaida siku hizi. Lakini Biblia inatutia moyo tuzungumze kuhusu imani yetu kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje aelewe andiko hilo?
